

11>> Idadi ya mabwawa ya kunyweshea mifugo maji

Bil. 6.2/- kujenga mabwawa 11 kunyweshea maji mifugo

Na MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema serikali imepanga kujenga mabwawa 11 ya kunyweshea maji mifugo na visima virefu vitatu.

Ulega alisema hayo wilayani Kilindi mkoani Tanga, juzi, wakati alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa bwawa la maji la Kwekinkwembe lililopo wilayani humo.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha, ameridhia kuipatia sh. bilioni 6.2 kwa ujenzi wa mabwawa hayo.

Naibu Waziri Ulega, alisema kila sekta

nchini, imeguswa ikiwemo ya mifugo na kwamba, hakuna iliyeachwa nyuma, hivyo wafugaji watanufaika kwa kupata maji ya uhakika baada ya mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kunyweshea maji mifugo kukamilika.

"Rais Dk. Samia hakuna aliyemwacha pembeni, ndiyo maana amegusa wakulima mbegu za ruzuku, amegusa wafugaji mabwawa na majosho, hivyo hakuna aliyeachwa nyuma," alisema.

Alimtaka mkandarasi anayefanya shughuli za ujenzi wa bwawa hilo, kuhakikisha anatoa taarifa ya kila hatua ya ujenzi na kuacha nakala wilayani hadi ngazi ya kijiji kunapojengwa, taarifa ziwe wazi na akamilishe kwa wakati.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Abel Busalama, aliwataka wananchi wa Kijiji cha Kwekinkwembe, kuhakikisha bwawa hilo linalojengwa kwa thamani ya sh. milioni 504, mara litakapokamilika, walisimamie vyema liwe na tija kwao.

Alisema uongozi wa kijiji, utapaswa kuweka utaratibu mzuri wa namna ya kuitumia na kulingezea thamani kwa kuyafanyia pia maji hayo shughuli mbalimbali.

Naye, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji (CCWT), wilayani humo, Merieki Long'oni, alisema ni faraja kubwa kwao kwa namna serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa kuwasogezea huduma ya maji karibu na mifugo yao.

ZIARA



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akikagua maendeleo ya ujenzi wa Bwawa la Kunyweshea Maji Mifugo la Kwekinkwembe, wilayani Kilindi, Mkoa wa Tanga, mwishoni mwa wiki. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Waonya shughuli za uvuvi kuingiliana na njia za meli

Na Abela Msikula, Mwanza

WADAU wa usafirishaji katika ziwa Victoria wameiomba serikali ku-komesha shughuli za uvuvi katika njia za meli, kwa usalama wa vyombo hivyo.

Walisema hiyo ni moja ya changamoto kubwa zinazowakabili, kwani nyavu za uvuvi huingia katika baadhi ya vifaa vya meli na kusababisha uharibifu mkubwa.

Walitoa malalamiko hayo katika mkutano wa kupokea maoni na changamoto zinazowakabili (wadau), kwa ajili ya uboreshaji zaidi wa bandari za ziwa Victoria.

Mkutano huo uliandaliwa na Mamlaka ya Bandari nchini (TPA) mwishoni mwa wiki, kupitia kamati yake ya maboresho ya bandari (PIC) ambapo mwakilishi wa Kampuni ya Kamanga Ferry, Mande Mangapi, alisistiza kwamba:

"Uwepo wa wavuvi katika njia za meli unaathiri utendaji kazi wetu kwa kiasi kikubwa, kwa sababu nyavu zao zinaingia katika 'propela' na kukondesha 'shafti', hivyo kutupa hasara kubwa."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Msaidizi wa Kampuni ya Mohamed and Brothers, maarufu kama 'Nyeheunge Express' Anwar Said, alipongeza jitihada za serikali kuboresha bandari lakini akashauri jitihada zaidi kufanyika ili kuufikia uchumi wa bluu mapema iwezekanavyo.

Alisema kote duniani hakuna biashara inayokua haraka tofauti na ya uchumi wa bluu pale uwekezaji katika rasilimali maji unapokua wa tija, akazishauri mamlaka zote husika nchini, ikiwemo ya uvuvi, kushirikiana katika matumizi ya rasilimali hizo ili Tanzania ifikie uchumi huo.

"Bahari na maziwa ndio uchumi wa bluu ambao ukuaji wake unategemea sekta hii ya maji ambayo inajumuisha usafiri nafuu, wenye uhakika na usalama zaidi.

"Kwa hiyo tunaipongeza serikali kwa kuchukua hatua madhubuti za kuongeza vyombo vya usafiri wa njia ya maji na kuweka mazingira yanayovutia wawekezaji wengi katika sekta hii ya uchukuzi.

"Hatua hii inayohusisha upanuzi wa bandari kote nchini inarahisisha biashara kati yetu na nchi jirani, hivyo kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Allon Kisaka, alisema hoja ya wavuvi imepokelewa kama sehemu ya maoni ya mkutano huo na itafikishwa katika mamlaka husika.

KANDA YA ZIWA

Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Kagera, Shinyanga



Na Nashon Kennedy,
Mwanza

MENEJA Mradi wa meli ya kihistoria kujengwa kwa ukanda wa ziwa Victoria na katika nchi za maziwa makuu ya Mv Mwanza Hapa Kazi Tu, Vitus Mapunda amesema meli hiyo yenye manufaa makubwa ya kiuchumi kwa nchi za maziwa makuu ina uhai wa zaidi ya miaka 50.

Mapunda aliyasema hayo jijini juzi katika mahojiano maalumu na HabariLEO juu ya umuhimu wa meli hiyo hapa nchini kwa sekta ya usafirishaji wa majini na ukuaji wa uchumi utokanayo

‘Meli ya Mv Mwanza ina uhai wa zaidi ya miaka 50’

na meli hiyo.

Alisema hiyo ni meli kubwa ambayo imejengwa kwa kuzingatia viwango vya ubora wa kimataifa ikiwa kwa usimamizi wa Taasisi ya Kimataifa ya Llodys kutoka Muungano wa Taasisi za Usimamizi wa Ujenzi wa Meli duniani (IACS).

“Tanzania tuna kila sababu ya kujivunia kukamilika

kwa ujenzi wa meli hii kwa pia viwango vya usalama ake vimezingatiwa,” alisema.

Aidha Vitus aliushukuru uongozi wa Chuo Kikuu cha Aalefund kutoka serikali ya kifalme ya Norway kwa kuwasomesha wahandisi watatu wa Kitanzania kwa kuwapatia udhamini wa mafunzo (Scholarship) katika kipindi cha miaka 20 iluyopita aki-

wemo yeye mwenyewe.

Aliwataja wahandisi wengine waliopata fursa hiyo kuwa ni pamoja na Abdallah Karume na Hassan Mfumi kwa kuwawezesha kupata ufadhili huo ambao ndio uliowawezesha kuwa miongoni mwa Watanzania waliosimamia na kujenga mradi huo mkubwa wa meli hiyo ya kihistoria.

Aidha, Vitus aliwashukuru Prof Arne Jan Sollied, Prof Vilmar na Mhandisi Gunner Nybo ambao amekuwa akiwasiliana nao mara kwa mara wakati wote wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa meli hiyo ya Mv Hapa Kazi tu.

Alisema meli hiyo ili-ajiri wakandarasi wazawa 17 wakiwemo wahandisi watatu

wa serikali huku ikitoa ajira kwa wachomoleaji, fundi bomba na waunganishaji vyumba zaidi ya 200 ambao wote ni Watanzania.

Alisema hatua inayofuata mara baada ya kushushwa kwa meli hiyo majini, ni kukamilisha ujenzi wa sehemu ya kukaa abiria, mfumo wa umeme na vifaa vya kuongezea meli hiyo.

presented the Tanzania country's sugar sufficiency by stands at 350,000 tonnes.
Authority (TPA) manag- 2025 The new plant will en- KSCL is the leading sugar

THE GUARDIAN

Page 3

By Guardian Report-

President Samia issues 6.2bn/- for building dams countrywide

er, Kilindi

PRESIDENT Samia Suluhu Hassan has agreed to disburse 6.2bn/- for the construction of water reservoirs for livestock across the country in this financial year.

Livestock and Fisheries deputy minister, Abdallah Ulega said here yesterday when inspecting construction progress of Kwekinkwembe dam located in Kilindi District, Tanga Region.

"President Samia is determined to improve every sector in the country, that's why she agreed to release such a huge amount of money to build dams that will provide water for livestock all over the country," Ulega said. Ulega said that every sector in the country has been affected, including livestock, and that no

one has been left behind, and so pastoralists will also benefit from getting reliable water once the dam construction project is completed. "Under President Samia, no one will be left behind, that's why she has touched farmers with subsidized fertiliser and improved seeds," the deputy minister said.

He however asked the contractor building the Kwekinkwembe dam to make sure he gives information on every step of the construction and left a copy in the district up to the village level where the dam is being built so that the information is clear and asked him to complete the construction on time.

Abel Busalama, Kilindi district commissioner has urged the peo-

ple of Kwekinkwembe village to ensure that the dam which is being built at a cost of 504m/- once it is completed, they manage it well so that it benefits them.

He said the leadership of the village of Kwekinkwembe will have to put in place a good system of how to use it and increase its value by also doing various agricultural activities.

THE UNITED REPUBLIC MINISTRY OF WORKS, TRANSPORT AND INFRASTRUCTURE

Telephone: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
E-mail: ps@mow.go.tz
Web site: www.mwtc.go.tz
In replay please quote:



PUBLIC NOTICE

PUBLIC NOTICE

Reco Engineering Company Ltd located in Chang'ombe Dar Es Salaam announces to Individuals and companies who brought their work to us and have not come to pick it up for a long time despite the several reminder but all ended in vain that they should come to pick up their work within one week from the date of this announcement else the company will not be responsible for the loss of property or any damage arising after this announcement.

Kindly note that when you are coming to take your property you have to bring copy of customer order for property verification subsequently the storage cost will be applied.

1. The general public is hereby movement of special load from Dar es Salaam to Nangurukuru, Lindi, Masasi, and Mtwara vehicle with registration number T 785 DYI / T 153 CHN

Of Mainline Carriers Ltd. The journey starts on 23rd February 2023

2. Special load dimensions:
Length - 18m
Width - 5.55m
Height - 4.80m

3. Route: From Dar es Salaam to Nangurukuru, Lindi, Masasi, and Mtwara be only day time (06:30 am - 06:00 pm)

We regret for any inconvenience